**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA KIBAHA**

**SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI**

**S.L.P 30267, KIBAHA–PWANI**

**NAMBA ZA SIMU : MKUU WA SHULE : 0716-604 438**

**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0759-929126/0656-765343/0658-460155**

KUMB. NA.MWASS/A.L/V.1/………………………………….

MZAZI/MLEZI WA:……………………………………………

S.L.P ………………….

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI KIDATO CHA TANO MWAKA ……….**

**UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Mwanalugali iliyopo Kibaha mkoa wa Pwani kwa mwaka wa masomo 20 tahasusi (combination) ya PCM/HGL/HGLi. Muhula wa masomo utaanza tarehe 04/07/2026 anatakiwa kuripoti shuleni kabla ya saa 11 jioni bila kukosa akiwa amevaa nguo ya heshima. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………..

**JINSI YA KUFIKA SHULENI**

Shule ya sekondari Mwanalugali ni shule ya Bweni ya wavulana, ipo umbali wa kilometa nne (4km) kutoka mailimoja Sheli, kushoto mwa barabara kuu itokayo Dar es Salaam kuelekea mikoani. Ukipanda basi toka mikoani shuka maili moja stand kuu ya mabasi (Kibaha), usafiri wa kukufikisha shuleni ni usafiri wa pikipiki ambao unagharimu Tshs. 4,000/=.

Fomu zote zilizoambatanishwa na maelezo haya zinatakiwa kujazwa kikamilifu.TUNASISITIZA FOMU HII KURUDISHWA BILA KUPUNGUZWA KURASA YOYOTE, ni mategemeo yetu kuwa mtasoma (Mzazi/Mlezi na Mtoto) kwa makini na kuzielewa.

**MICHANGOYA SHULE**.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizi zilipwe kwenye akaunti ya shule NMB A/C Na. 21201200150 jina la akaunti ni MWANALUGALI SECONDARY SCHOOL RECURRENT. Mwanafunzi aje na pay in slip shuleni siku anayoripoti ikionyesha jina kamili la mwanafunzi na tahasusi yake. Hakikisha unabaki na nakala moja ya bank pay in slip.

**NB.MALIPO YOTE YA SHULE YALIPWE BANK HATUPOKEI PESA TASLIMU ZA MICHANGO YA SHULE ILIYOORODHESHWA HAPO JUU KATIKA JEDWALI.**

## 2.0 SARE YASHULE

- Suruali mbili rangi ya **Light Grey (**Esteem No 1**)** kitambaa cha suti zilizoshonwa na selebration (marinda mawili) yenye upana inch 14 na turn up, ziwe zimeshonwa kwa heshima na zisiwe za kubana (MODAL) kwa ajili ya darasani, na suruali moja ya **Dark**blue (Esteem No 1**)** (unaweza kuja kushona shuleni) kwa ajili ya kushindia na kazi za nje, haya ndio yatakuwa mavazi yake kipindi chote atakachokuwa shuleni, hataruhusiwa kuvaa nguo za nyumbani.

- Shati mbili nyeupe mikono mirefu.
- Tai rangi ya **Light grey (satin material)**
- Soksi **nyeusi** jozi 2 zisiwe na marembo
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba na Kisigino kifupi (visiwe buti)
- T-shirt mbili rangi ya **brown zenye nembo.**
- Sweta moja rangi ya **grey yenye nembo.**
- Tracksuit moja ya rangi ya **Light grey** yenye nembo kwa ajili ya masomo ya jioni (evening preparation).
- Jezi ya Taifa Stars **(Rangi Nyeusi)**

NB: SARE ZINAPATIKANA SHULENI

## 2.1 MAHITAJI MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

- Bunda(ream la karatasi **A4**) mbili kwa mwaka.
- Faili moja (1) (Linapatikana Shuleni).
- Madaftari makubwa counter books Nane(8).
- Mathematical set, scientific calculator (**fx991,2wayPower)** kwa watakao soma geography na mchepuo wa sayansi.
- Oxford advanced learner’s dictionary moja(1) kwa watakaosoma masomo ya

lugha.

- Kalamu za blue na nyeusi za kutosha na penseli.
- Vifaa vya michezo raba.
- Shukambili (2) za **lightblue** na chandarua cheupe.
- Mto na foronya za **light blue.**
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na sabuni za kutosha za mche na za unga.
- Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe, kijiko vyote vya **aluminium**(Bati).
- Godoro la futi mbili na nusu kwa sita ($2^{1/2}$x6).
- Sanduku la bati na kufuliza kufungia sanduku lake.
- Ndoo ndogo mbili(2) zenye mfuniko rangi ya blue au nyekundu.

- Vifaa vya usafi: kila mwanafunzi alete vifaa vya usafi kama ilivyoainishwa hapa chini kwa kila tahasusi;-

1. PCM: Fagio la nje, kwanja, rubber squeezer na Toilet Brush.
2. HGL: Softbroom, reki1, hardbroom na rubber squeezer.
3. HGLi: Mopper 2, Fagio la nje na koleo (chepe)
4. Kila mwanafunzi aje na vitabu muhimu kulingana na masomo anayosoma (vitabu vya TIE).
5. Mwanafunzi **haruhusiwi** kuja na **simu ya mkononi, heater, jagi la kuchemshia maji hapa shuleni/bwenini**.
6. Kila mwanafunzi aje na **kadi ya bima ya afya (NHIF)** kwa ajili ya matibabu (kama hana Bima aje na Fedha kiasi cha **Tsh.51000/-).**

**NB : TUNASISITIZA KUZINGATIA MAELEKEZO HAYA.**

NAKUTAKIA KILA LA KHERI NA KARIBU MWANALUGALI SEKONDARI.

…………………

UYEKA KESSY MRISHO

**MKUU WA SHULE.**

**SHERIA ZA SHULE**

Katika jamii yoyote ile ni lazima kuwepo na SHERIA, KANUNI NA TARATIBU zitakazowezesha jamii hiyo kuishi kufuata maadili mema na mazuri ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**1. MAHUDHURIO**

i. Wanafunzi wote wawapo shuleni ni lazima waisome,waielewe na waifuate kwa makini ratiba ya shule ya kila siku.
ii. Kwa kuwa lengo ni kupata elimu, wanafunzi wote ni lazima wahudhurie na kuwahi vipindi vya darasani, vipindi vya elimu ya kujitegemea na vipindi vya michezo na shughuli zingine zozote za shule kama zitakavyopangwa katika ratiba, isipokuwa ruhusa ya kutokuhudhuria itatolewa.
iii. Pia mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa kukimbia/kutohudhuriana kutofanya mitihani
iv. Pia mwanafunzi hatoruhusiwa kutoka nje ya mazingira ya shule bila ya kibali maalumu kitakachotolewa na mwalimu wa zamu au mlezi.
v. Wanafunzi wote wanatakiwa kufuata ratiba ya shule ya siku kwa usahihi kuanzia 1:10 asubuhi mpaka saa 4:30 Usiku au kama itakavyoeleza vinginevyo.
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kushiriki kikamilifu shughuli zote baada ya ratiba ya darasani kama elimu ya kujitegemea, clubs, mdahalo, michezo, na usafi wa mazingira.

**2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria Vipindi vya darasani;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kukutwa bwenini Muda wa Darasani;
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
viii. Kufuga ndevu;
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
x. Uvutaji wa sigara na Bangi;
xi. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera yaTaifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**NB**: **UPOTEVU AMA UHARIBIFU WA VIFAA VYA SHULE VITALIPWA NA MHUSIKA KWA GHARAMA HALISI YA VIFAA HIVYO AU KIFAA CHENYEWE.**

**3. HESHIMA**

i. Wanafunzi wote wanatakiwa kutii kengele
ii. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa kwa unadhifu na usahihi na kuchomekea wakati wowote wanapokuwa katika sare ya shule. ATAKAYEVAA MODAL/BWANGA ITAKATWA NA KUTEKETEZWA ILI KULINDA HESHIMA NA MAADILI YA TAIFA. (Tunasisistiza Heshima katika mavazi).
iii. Wanafunzi wote wanatakiwa kusimama paredi kwa unadhifu na ukakamavu
iv. Wanafunzi wasimame kusalimia walimu au mgeni aingiapo darasani
v. Wanafunzi wasitoke darasani bila ruhusa na kwa makundi makundi
vi. Wanafunzi wasipige kelele darasani
vii. Wanafunzi waheshimiane wao kwa wao na waheshimu viongozi
viii. Hairuhusiwi kupiga mayowe darasani au nje ya darasa
ix. Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni pamoja na maeneo jirani yanayozunguka shule.
x. Wanafunzi wawe katika mfano bora katika fani zote, heshima, kazi na usafi hata wanapokuwa nje ya mazingira ya shule.
xi. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi na nadhifu
xii. Wanafunzi hawaruhusiwi kufuga ndevu.

**4. MIPAKA YA SHULE**

i. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali. Wanafunzi hawataruhusiwa kutoka nje ya maeneo ya shule mara watakapopokelewa shuleni mpaka shule itakapofungwa au kibali maalum kama kwenda kanisani, msikitini na hospitali kwa muda maalum , pia wanafunzi hawaruhusiwi kufika sehemu zifuatazo isipokuwa kwa ruhusa maalum.

   a. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasiowalimu
   b. Ofisi zote za shule bila sababu maalum
   c. Maabara bila sababu maalum
   d. Jikoni

ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika sehemu zifuatazo.
   a. Vilabu vyote vya pombe
   b. Majumba ya kufikia wageni
   c. Majumba ya starehe
   d. Makazi ya **watu(majirani)** bila ruhusa au sababu maalum

**5. CHAKULA**

- Chakula cha wanafunzi kitapatikana shuleni, shule haitoi chakula maalum (**hakuna special Diet)** kwa wanafunzi wenye shida, wanafunzi wote watakula chakula kilicho idhinishwa na shule.

## 6. MABADILIKO YA MAJINA NA ANUANI

i. Endapo jina na anuani ya mzazi/mlezi vitabadilishwa kwa sababu yoyote taarifa itolewe shuleni ili rekodi za shule ziwe sahihi wakati wowte na hasa wakati wa kupokea taarifa mbalimbali kwa mzazi/mlezi kuhusu maendeleo ya mwanafunzi.

ii. Majina ya wanafunzi yaliyopokelewa shuleni ndiyo yatakayotumika bila kubadilishwa

NB: Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA**

....................

UYEKA M. KESSY

**MKUU WA SHULE**

## 7. TAARIFA KUHUSU MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI

Ndugu Mzazi/Mlezi……………………………………………

Shule inapenda kufahamu mambo yafuatayo kuhusu mtoto wako

1. Jina Kamili ……………………………………………
2. Tarehe yake ya kuzaliwa………………………………
3. Kabila lake……………………………………………
4. Dini yake………………………………………………
5. Mahali alipozaliwa……………………………………
6. Je, ana ugonjwa wowote unaomsumbua mara kwa mara NDIO/ HAPANA kama ndio anatibiwa hospitali ipi?...............................
7. Je, anashida yoyote kimaumbile au kiafya?................................
8. Anaishi na nai nyumbani Mzazi/Mlezi, kama ni mlezi ana uhusiano gani na mtoto?..........................................
9. Jina la Mzazi/Mlezi……………………………….

   Anuani yake………………………………………

   ………………………………………

   ………………………………………

   Simu yake kazini………………………………………

   Simu yake ya nyumbani………………………………

   Kazi ya Mzazi/Mlezi…………………………………

**HALMASHAURI YA MJI KIBAHA**
**SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI**
**S.L.P 30267 – KIBAHA**
**AHADI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANALUGALI**

1. Jina la Mwanafunzi………………………………………….
2. Jina la Kijiji au mtaa atokako…………………………………..
3. a) Jina na anuani ya mzazi/mlezi na namba ya simu
   ……………………………………………………….

   ……………………………………………………...

   ……………………………………………………...

   b) Jina na anuani ya ndugu wengine wanaohusika katika kufuatilia nidhamu ya mtoto. (Dada, Kaka, Majomba) andika namba ya simu kama ipo.

   i)……………………………………………….
   ii)………………………………………………
   iii)……………………………………………..
4. Mimi (jina la Mwanafunzi) ……………………………………… Nimekubali/sijakubali kujiunga na jumuiya ya shule ya secondary Mwanalugali, wakati wote naahidi kuwa mtiifu kufuata na kuzingatia taratibu za shule, kutunza mali ya umma na kufanya kazi kadri ya uwezo wangu na juhudi na maarifa.

5. Nafahamu kwamba kitendo chochote kilicho kinyume na mwenendo na utaratibu wa shule kinastahili adhabu kali kama itakavyoamuriwa na jumuiya ya shule pamoja na bodi ya shule.

6. Nimeyaona maagizo yote nimeyasoma na kuyaelewa

   Sahihi:……………………… Tarehe……………………

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
**STUDENTS NAME: ……………………………………………………………………**
(To be completed by a Government Medical Officer). I have examined the above-named students and consider that she /he is fit/unfit for a full-time studies.

i) Euesogit……………………………………………………………………

ii) Hearing……………………………………………………………………

iii) Speech…………………………………………………………………..

iv) Limbs……………………………………………………………………

v) General disease………………………………………………………….

vi) Leoprosy…………………………………………………………………

vii) Epilepsy…………………………………………………………………

viii) Neurosis…………………………………………………………………

ix) Other serious diseases e.g. Asthma…………………………………………

x) TB……………………………………………………………………...

xi) Pregnancy…………………………………………………………………

xii) Abdomen…………………………………………………………………

xiii) Urinalysis…………………………………………………………………

xiv) Hemoglobin (blood examination) ……………………………………………

Comment……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
………………………………………………………………

**Date…………………………** **Signature…………………**

**STATION……………………………….** **Designation**……………….

………………………..

UYEKA M. KESSY

HEADMASTER